
MWONGOZO WA ENEO LA MIGOGORO KWA WATAFSIRI/WAKALIMANI WA KIRAIA NA WATUMIAJI WA HUDUMA ZAO



www.aiic.org



www.fit-ift.org



www.red-t.org

Watafsiri na wakalimani waliopewa kandarasi ya kufanya kazi katika maeneo ya migogoro mara nyingi ni wanaisimu wasio wataalamu lakini bado wana jukumu muhimu katika mawasiliano. Wanafanya kazi katika mazingira inayohatarisha maisha yao na wanahitaji ulinzi maalum wakati na baada ya migogoro. Watumiaji wa huduma za watafsiri na wakalimani lazima wafahamu wajibu wao kwa watafsiri na wakalimani wa kuwalinda. Wakati huo huo, watafsiri na wakalimani wenyewe sharti wajue haki zao pamoja na kuzingatia viwango na maadili ya taaluma ya lugha ili kuimarisha usalama na msimamo wao.

Hati hii ni mwongozo wa haki, wajibu, na mazoea ya msingi ambayo Chama cha Kimataifa cha Wakalimani wa Mikutano (AIIC), Shirikisho la Kimataifa la Watafsiri (FIT), na Red T zinapendekeza kwa watafsiri na wakalimani na watumiaji wa huduma zao. Inatumika na watafsiri na wakalimani wanaofanya kazi kama wataalamu wa lugha kwa vikosi vya jeshi, waandishi wa habari, mashirika yasiyo ya kiserikali, na mashirika mengine katika maeneo ya migogoro.

KWA WATAFSIRI NA WAKALIMANI

HAKI

Ulinzi

Una haki ya kulindwa wakati na baada ya kazi. Ikiwa ni lazima, hii inapaswa kujumuisha familia yako pia. Unapaswa kupewa mavazi na vifaa vya kujikinga, lakini sio silaha. Kama raia, hutakiwi kuvaa sare isipokuwa kwa idhini yako. Msaada wa matibabu na kisaikolojia lazima uwepo kwako. Kabla ya kupangwa kikazi, unapaswa kupewa mafunzo ya usalama na dharura.

Msaada

Una haki ya kupata msaada wakati wote wa kazi yako, kwa mfano, bidhaa za kibinafsi na vifaa vinavyofaa kwa eneo la kazi au kituoni.

Mipaka

Mipaka ya jukumu lako lazima ielezwe wazi. Una haki ya kukataa kazi ambayo inaathiri viwango na maadili yako ya kitaaluma au ya kibinafsi na / au inahatarisha usalama wako.

Maagizo ya awali

Unapaswa kufahamishwa kuhusu muktadha wa jumla na maalum kwa kazi yako.

Hali

Una haki ya kulipwa na vifungu vingine vya mkataba vinavyozingatia mazingira inayohatarisha maisha yao. Masaa ya kazi yanapaswa kuwa adilifu na kupata mapumziko ya mara kwa mara.

MAJUKUMU

Kutopendelea

Bila kujali ni nani anayekushirikisha, tumikia pande zote kwa usawa bila kuonyesha maoni au huruma zako. Huwezi kuwa mtetezi wa sababu yoyote na lazima utangaze mgongano wowote wa maslahi.

Usiri

Hifadhi hali ya siri ya habari yoyote unayopata kutoka kwa upande wowote wakati wa kazi yako. Usiifichue kwa mtu yeyote au kuitumia kwa manufaa ya kibinafsi.

Usahihi

Wasilisha kwa uaminifu iwezekanavyo ujumbe wa pande zote. Ili kufanya hivyo...

- Jifunze stadi za msingi za ukalimani, yaani, sikiliza kwa makini kile kinachosemwa, kitafsiri kwa uwazi katika lugha hiyo nyingine, na uwe makini kwa tofauti za kitamaduni pamoja na ishara zisizo za maneno.
- Jiandae kwa kazi kwa kujifunza msamiati maalum, vifupisho, istilahi, n.k., na ujifahamishe kwa lafudhi, ishara, desturi, n.k.
- Andika vidokezo kama vitakusaidia kukumbuka.
- Usikague au kurekebisha taarifa zilizowasilishwa na wazungumzaji.
- Ikibidi, omba ufafanuzi, omba mzungumzaji apunguze kasi, au onyesha ishara kwa mzungumzaji kama haeleweki.

KWA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA WATAFSIRI NA WAKALIMANI

HAKI

Una haki ya tafsiri/ukalimani sahihi ya ujumbe wako. Kwa kutimiza majukumu yaliyoorodheshwa hapa chini, utasaidia watafsiri na wakalimani katika kufikia lengo hilo.

MAJUKUMU

Heshima

Watafsiri na wakalimani ni kiungo kati yako na watu wa nchi ambayo unafanya kazi. Heshimu watafsiri na wakalimani na watakuheshimu. Cheo kinaweza kuanzishwa lakini sio kutumiwa vibaya.

Ulinzi

Watafsiri na wakalimani wanaweza kuwa hatarini wanapokufanyia kazi. Ikiwa unawajibika kimkataba au la, uwalinde na, ikiwa ni lazima, familia zao pia wakati wa kazi na baadaye.

- Usiwape silaha.
- Wapatiwe mavazi na vifaa vya kujikinga, lakini usiwahitaji kuvaa sare isipokuwa kwa idhini yao.
- Usitoe majina, anwani, au picha za watafsiri na wakalimani bila idhini yao.

Msaada

Saidia watafsiri na wakalimani wako kwa kuwapa bidhaa za kibinafsi na vifaa vinavyofaa kazini na kituoni. Kuwa na ufahamu wa mahitaji na wasiwasi wao.

Ufafanuzi wa jukumu

Fafanua wazi jukumu la watafsiri na wakalimani. Eleza masharti ya uendeshaji na mnyororo wa shughuli za uwajibikaji. Kwa ujumla, usiwapatie kazi zisizohusiana na utafsiri / ukalimani, na ujue kuwa watafsiri na wakalimani wana haki ya kukataa ikiwa kazi hiyo inaathiri viwango vya kitaaluma au vya kibinafsi na maadili na / au usalama wao.

Mipango

Ukalimani unahitaji umakini, ambayo ni vigumu kudumisha katika hali ya mgogoro. Kubaliana juu ya masaa ya kazi, mapumziko, n.k. Wakati wa kutumia huduma za watafsiri na wakalimani, zingatia muda wa ziada na mahitaji mengine ya usafiri.

Maagizo ya awali

Toa maagizo kwa watafsiri na wakalimani kwa ujumla na hasa kabla ya kila kazi kuhusu muktadha na madhumuni. Eleza msamiati maalum, vifupisho, istilahi, n.k.

Tathmini

Ikiwa inahitajika kutathmini utendaji wa mtafsiri na mkalimani, kuwa wa haki na kutumia mfumo sahihi wa tathmini. Fuatilia ikiwa ujumbe unawasilishwa kwa usahihi, lakini elewa kwamba ukalimani sio neno kwa neno na kwamba ujumbe wako wa awali lazima uwe wazi. Ukosoaji unapaswa kufanywa kwa faragha. Zawadi, mapendekezo, n.k. zinapaswa kutolewa pale inapostahili.

JINSI YA KUFANYA KAZI NA WATAFSIRI NA WAKALIMANI

Nafasi

Jiweke mwenyewe, mtafsiri na mkalimani, na mhusika huo mwingine katika umbo la pembe tatu. Hakikisha kwamba wewe, mtafsiri na mkalimani, na mhusika huo mwingine nyote mnaweza kuangaliana na kusikilizana. Jitambulisha pamoja na mtafsiri na mkalimani, ukielezea jukumu la mtafsiri na mkalimani. Ongea na uangalie mhusika huo kingine, sio mtafsiri na mkalimani.

Kuzungumza

Mtafsiri/mkalimani anasubiri uzungumze na kutafsiri unapotulia. Kiasi cha habari ambacho mtafsiri na mkalimani anaweza kukumbuka na kusema kwa usahihi hutegemea kiwango chake cha ujuzi.

- Tumia maneno rahisi na sentensi fupi, zenye mantiki.
- Ongea kwa uwazi na sio haraka sana.
- Jaribu kuepuka misimu, vifupisho, istilahi, au marejeo yasiyoelweka katika utamaduni mwingine.
- Kumbuka kuwa ucheshi, ingawa unasaidia katika kupunguza mvutano, ni vigumu kuutafsiri.
- Kuwa na ufahamu wa lafudhi, lahaja, na muundo wako wa hotuba, na jinsi zinavyoweza kuathiri kazi ya utafsiri na ukalimani.
- Kuwa na ufahamu wa kile unachosema na jinsi unavyosema.

Kukagua

Una jukumu la kuhakikisha kuwa ujumbe unaeleweka na pande zote. Kama hujaelewa mhusika huo mwingine amesema nini, mwombe arudie na/au afafanue. Kama unadhani mhusika huo mwingine hajaelewa ulichokisema, thibitisha kuwa mtafsiri na mkalimani amekuelewa. Hata hivyo, epuka kufanya mazungumzo ya faragha na mtafsiri na mkalimani isipokuwa kama mhusika huo mwingine anajua kwa ujumla unachojadili.

Udhibiti

Usikabidhi jukumu kwa watafsiri na wakalimani. Hawapaswi kutoa tamko au kuuliza swali kwa niaba yako; wanatafsiri tu kile unachosema. Endelea kudhibiti mazungumzo, lakini tafuta ushauri wa mtafsiri na mkalimani pale inapobidi na inapofaa.